# TANGAZO LA ZABUNI

## HALMASHAURI YA WILAYA YA KIGOMA

KIGOMA DISTRICT COUNCIL
P. O. Box 332

TAREHE: 18/10/2023

### ZABUNI ZA VYANZO MBALIMBALI VYA MAPATO YA HALMASHAURI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

1.0 Halmashauri ya wilaya ya Kigoma inapenda kuwaalika watu binafsi, makampuni,mashairika, Taasisi au Vikundi vilivyosajiliwa kisheria vyenye nia na uwezo wa kufanya uwakala wa kukusanya mapato kwenye vyanzo mbalimbali vya mapato ya Halmashauri kwa kipindi cha kuanzia **Oktoba 24, 2023** hadi **Novemba 7, 2024**

2.0 Zabuni mbalimbali zilizopo ni kama ilivyoainishwa hapa chini:-

| NA | CHANZO/MAHALI | MAELEZO YA CHANZO | NAMBA YA ZABUNI |
|---|---|---|---|
| 1 | MATENDO SOKONI | USHURU WA TANGAWIZI,USHURU WA SOKO NA BIDHAA ZOTE | LGA/043/20223/2024/NC/REV/01 |
| 2 | PAMILA SOKONI | USHURU WA SOKO NA BIDHAA ZOTE | LGA/043/20223/2024/NC/REV/02 |
| 3 | KIDAHWE SOKONI | USHURU WA MKAA,TANGAWIZI,VIAZI NA USHURU WA SOKO NA BIDHAA ZOTE | LGA/043/20223/2024/NC/REV/03 |
| 4 | MACHAZO STENDI | USHURU WA MAEGESHO YA DALADALA NA MAZAO MBALIMBALI | LGA/043/20223/2024/NC/REV/04 |
| 5 | KASUKU RELINI | USHURU WA MKAA,KUNI,MISE,MAWESE,NYANYA NA BIDHAA ZOTE | LGA/043/20223/2024/NC/REV/05 |
| 6 | KASUKU SOKONI | USHURU WA SOKO NA BIDHAA ZOTE | LGA/043/20223/2024/NC/REV/06 |
| 7 | SIMBO SOKONI | USHURU WA SOKO NA BIDHAA ZOTE | LGA/043/20223/2024/NC/REV/07 |
| 8 | KASEKE YA CHINIZIWANI | USHURU WA MAZAO YA UVUVI NA BIDHAA ZOTE | LGA/043/20223/2024/NC/REV/08 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 9 | MUNGONYA MATOFALINI | USHURU WA MATOFALI NA BIDHAA ZOTE | LGA/043/20223/2024/NC/REV/09 |
| 10 | MAHEMBE NJIAPANDA | USHURU WA MAWESE,MISE, NA BIDHAA ZOTE | LGA/043/20223/2024/NC/REV/10 |
| 11 | KIZENGA NJIAPANDA | USHURU WA MAWESE, MISE,MKAA, NA BIDHAA ZOTE | LGA/043/20223/2024/NC/REV/11 |
| 12 | MWANDIGA STENDI | USHURU WA MAEGESHO YA MAGARI | LGA/043/20223/2024/NC/REV/12 |
| 13 | BITALE SOKONI | USHURU WA SOKO,MKAA NA BIDHAA ZOTE | LGA/043/20223/2024/NC/REV/19 |
| 14 | KALINZI SOKONI | USHURU WA NANASI,NDIZI,USHURU WA SOKO SOKO NA BIDHAA ZOTE | LGA/043/20223/2024/NC/REV/21 |
| 15 | NYARUBANDA SOKONI | USHURU WA NANASI, NDIZI, USHURU WA SOKO NA BIDHAA ZOTE | LGA/043/20223/2024/NC/REV/22 |
| 16 | MKIGO SOKONI | USHURU WA MBAO, NANASI, NDIZI USHURU WA SOKO NA BIDHAA ZOTE | LGA/043/20223/2024/NC/REV/23 |
| 17 | KILEMBA MACHIMBONI | USHURU WA PEMBA, NA BIDHAA ZOTE | LGA/043/20223/2024/NC/REV/24 |
| 18 | KAMALA SOKONI | USHURU WA MAWESE,USHURU WA SOKO NA BIDHAA ZOTE | LGA/043/20223/2024/NC/REV/25 |
| 19 | BUBANGO SOKONI | USHURU WA SOKO, MAWESE, MISE, NA BIDHAA ZOTE | LGA/043/20223/2024/NC/REV/26 |
| 20 | MWAMGONGO WALONI NA SOKONI | USHURU WA MAZAO YA UVUVI, USHURU WA SOKO NA BIDHAA ZOTE | LGA/043/20223/2024/NC/REV/28 |
| 21 | ZASHE | USHURU WA MAZAO YA UVUVI NA BIDHAA ZOTE | LGA/043/20223/2024/NC/REV/29 |
| 22 | MGARAGANZA | USHURU WA TOFALI,MAWESE, MISE, NA BIDHAA ZOTE | LGA/043/20223/2024/NC/REV/32 |
| 23 | GETI LA SIMBO | USHURU WA MIZIGO NA MALIASILI | LGA/043/20223/2024/NC/REV/33 |

NB: BIDHAA ZOTE NI ZILE ZILIZOAINISHWA KWENYE SHERIA NDOGO ZA HALMASHAURI YA KIGOMA

## 3.0 MASHARTI YA MAOMBI YA ZABUNI

1. Mwombaji zabuni alipe ada ya zabuni ya sh. **30,000/=** ambazo hazitarudishwa kwa kila zabuni atakayoomba.
2. Mwombaji ataje kiasi ambacho atalipa kwa mwezi kwa zabuni atakayoomba
3. Mwombaji anaruhusiwa kuomba zabuni zaidi ya moja kulingana na uwezo wake.

4. Mwombaji ambaye ni mtu binafsi anatakiwa aambatanishe barua ya utambulisho ukazi wa kutoka kwa Afisa Mtendaji wa Kijiji, Kitongoji, mtaa au Kata pamoja na picha yake ya ukubwa wa passport. Aidha atatakiwa aambatanishe barua za wadhamini wake wawili na picha zao za ukubwa wa passport
5. Mwombaji ambaye ni kampuni atatakiwa aambatanishe leseni ya biashara iliyohai, cheti cha usajili wa namba ya mlipa kodi **(TIN).** Aidha mwombaji ambaye ni kampuni anatakiwa kuwasilisha hati ya uwakilishi wa kisheria **(Registered special power of attorney)** na vielelezo vya kuonesha umiliki wa kampuni hiyo **(Memorandum na articles of association au extract from the register)**
6. Mwombaji ambaye ni kikundi awasilishe cheti cha usajili wa kikundi na barua ya kuwatambulisha Mwenyekiti na Katibu wa kikundi pamoja na picha zao za ukubwa wa passport.
7. Mwombaji asiwe mtumishi au kiongozi wa ngazi ya kisiasa wa Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma.
8. Mwombaji ambaye si raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania haruhusiwi kuomba zabuni hizi
9. Mwombaji wa mojawapo wa zabuni hizi anashauriwa kutembelea chanzo/vyanzo husika kabla ya kuomba ili kutaja kiasi atakachomudu kuilipa halmashauri kwa mwezi
10. Mwombaji wa zabuni hizi awe tayari kutumia **mashine za POS** katika kukusanya mapato ya Halmashauri na kutoa risiti za mashine ya POS. **Mashine za POS** zitatolewa na Hamashauri pamoja na maelezo ya namna ya kuzitumia kutoa risiti.
11. Mwombaji aandike juu ya bahasha na kwenye barua ya maombi aina na namba ya zabuni aliyoomba. Atatakiwa kutuma kabrasha halisi la maombi (original) pamoja na nakala kivuli yake (copy) ambazo zitawekwa ndani ya bahasha moja kubwa. Juu ya bahasha kusiandikwe wala kuwekwa alama yoyote zaidi ya **jina la zabuni, namba ya zabuni** na anwani ifuatayo:

**KATIBU WA BODI YA ZABUNI,**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA KIGOMA,**
**S.L.P 332, KIGOMA**

12. Maombi ya zabuni yawasilishwe kwenye Kitengo cha Usimamizi wa Ununuzi kilichopo kwenye ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya wilaya kando ya barabara ya Bangwe, Kigoma.

13. Mwisho wa kupokea maombi ni **tarehe 07/11/2023 Siku ya Jumanne** saa **tano kamili (5.00)** asubuhi. Maombi ya zabuni yatakayowasilishwa baada ya muda huo hayatapokelewa.
14. Bodi ya zabuni itakuwa na haki ya kuteua mwombaji ambaye amekidhi vigezo, hivyo haitalazimika kumchagua mwombaji mwenye makisio ya juu wala ya chini.

Jabili Timbako
Kaimu Mkurugenzi Mtendaji (w)
Halmashauri ya Wilaya,
**KIGOMA**

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
KIGOMA